

Mkakati wa Makazi wa NSW

Januari 2023 - Juni 2025



NSW Government's Settlement Strategy (Mkakati wa Makazi wa Serikali ya NSW) inalenga kuboresha matokeo ya makazi kwa wakimbizi wanaoishi katika NSW. Mkakati huu ni wa kwanza wa aina yake katika jimbo na Australia na unafanya kazi kufikia matokeo sita ya muda mfupi kwa wakimbizi na jamii.



Wakimbizi wanapata huduma zinazofaa na taarifa ambazo wanaweza kuelewa na kushirikiana nazo



Upangaji na tathmini (evaluation) ya makazi ya Serikali ya NSW inaarifiwa na mambo yaliyo onwa



Wakimbizi wana fursa na msaada ku shiriki kijamii na/au kiuchumi



Serikali ya NSW imeboresha michakato ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa ili kusaidia upangaji wa makazi unaotegemea ushahidi



Mitandao inayotegemea mahali na ya jumuiya imejumuishwa katika upangaji wa makazi, ikiwa ni pamoja na kukaribisha watu katika jumuiya



Serikali ya NSW imeongeza ushawishi katika kufanya maamuzi ya kitaifa kuhusu shabaha za makazi, sera (policy) na matokeo

Mkakati huu unatambua mfumo tata (complex) wa makazi uliopo katika NSW na matokeo ya muda mrefu ambayo yanahitaji ngazi zote za serikali na sekta isiyo ya serikali kufanya kazi pamoja ili kufikia.

NSW Settlement Strategy (Mkakati wa Makazi wa NSW) inalenga hasa wakimbizi ambao wako ndani ya miaka 10 ya kwanza ya safari yao ya makazi na wanaoishi NSW.

Kwa madhumuni (miradi) ya Mkakati wa Makazi wa NSW, neno 'wakimbizi' linajumuisha watu wote kutoka asili kama wakimbizi, ikiwa ni pamoja na watu wanaotafuta hifadhi.

Mkakati huleta pamoja bidii ya mpia na ya zamani ya serikali ya NSW kwenye:

- Eleza nini maana ya Serikali ya NSW kwa safari za makazi na nini kinajumuisha makazi yenye mafanikio
- Pachika sauti ya mambo yaliyo onwa katika kufanya maamuzi
- Kuimarisha na kurasimisha ushirikiano, uratibu, mipango mkakati na utoaji wa huduma katika Serikali ya NSW
- Kuhakikisha uboreshaji endelevu, tathmini na kujenga uwezo katika Serikali ya NSW ili kuhakikisha matokeo ya makazi yenye mafanikio
- Shirikisha watendaji mbalimbali wa sekta mtambuka na jamii ili kuhakikisha wakimbizi wanastawi
- Kujenga na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati uliopo na Jumuiya ya Madola, Jimbo na Wilaya nyingine, na Serikali za Mitaa ili kushawishi ufanyaji maamuzi wa kitaifa

NSW Settlement Strategy (Mkakati wa Makazi wa NSW) inajumuisha:

Mpango wa Utekelezaji (Action Plan) ambao unaeleza jinsi Serikali ya NSW itaendelea na kuimarisha mipango iliyopo na kutekeleza mipango ya ziada ili kushughulikia mapungufu yaliyotambuliwa

Mfumo wa Tathmini (Evaluation Framework) ambao utasaidia Serikali ya NSW kufuatilia na kupima maendeleo na kuwa na taarifa ili kuweza kukabiliana na mahitaji yanayojitokeza katika NSW

NSW Settlement Strategy (Mkakati wa Makazi wa NSW) ni kipaumbele cha kimkakati kwa Multicultural NSW na inatekelezwa na Serikali ya NSW.